

Public education  
Discover a world of opportunities

# NAMBA: KUSOMEA NYUMBANI

## KUTAMBUA HESABU


Hapa ni baadhi ya mawazo ya kukusaidia kuweza kuleta hesabu katika maisha ya mtoto wako:

- Fikiria kwa upana wakati unatumia hesabu, wakati, nafasi na vipimo ili mtoto wako aone umuhimu wa hesabu. Kwa mfano: *Nashangaa kama tuna mapera ya kutosha? na tusumbili tuhesabu ili kuhakikisha.*
- Hamasisha mtoto wakoaweze kuzungumzia vitu anachofanya. Uliza maswali na ruhusu mtoto wako kuuliza maswali pia questi. Hii inasaidia kuelewa vitu kwa maana na kusaidia vile vinavyofanywa. Ni njia bora ya kusoma.
- Tumia hesabu na maneno ya namba wakati unafafanua vitu. Badala ya kusema: *Ndoo, unaweza kusema: Lita 10 (kumi) za maji.* Hii inasaidia mtoto wako kujifunza maneno mbalimbali yanayotumika kuelezea jinsi ya kupima vitu.

**Zima televisheni. Ni rahisi mtoto wako kuweka umakini kama hakuna vitu vingine vya kumhangaiisha.**

**Fuata sheria ya dhahabu ya 'kidogo na mara kwa mara– dakika chache kila siku akijifunza hesabu ni bora kuliko dakika 30 za hisabati.**

- Uliza mtoto wako maswali wakati wewe unafanya shughuli za kila siku ili waweze kuanza kufikiria na kuzungumzia kuhusu hesabu kuanzia umri mdogo. Uliza maswali kama vile: *Viko vingapi pale? Hii ni njia ipi? Je itaenea pale? Je vinatosha sisi wote? na ni ukubwa wa kiasi gani?*
- Mfanye mtoto wako akusaidie kuchambua vitu nyumbani kulingana na ukubwa, urefu, rangi na sura, kwa mfano vifungo, soksi, vigingi na vitalu.
- Msifie mtoto wako kwa kujaribu, hata kama jibu sio ya ukweli. Kama hawajui majibu, wape mda wa kutafakari. Kama ukiwambia jibu, waelezee jinsi ulivyolipata. Hii inajenga kujiamini kwa kusoma. Wape mda wa kufikiria na mda wa kujibu maswali yako. Uwe mvumilivu.



Department of  
Education

**Utakuta masomo zaidi kwenye  
Vifurushi vya habari za nyumbani  
kwenye [education.wa.edu.au](http://education.wa.edu.au).**